KWA JINA LA ALLAAH, MWINGI WA REHEMA, MWENYE KUREHEMU

Al-Hudaa [Uongofu]

الهدى

25/= Ksh

Volume 9, Issue 4

18th Jumâ al-Awwal 1432

22nd April, 2011

YALIYOMO

UZINIFU 1 - 3

GHULUW 3 - 4

MABAYA YANAYOPATIKANA KUTOKAMANA NA UZINIFU

Mtayarishi: SHEIKH MUHAMMAD IBRAHEEM AL-HAMAD

Twamshukuru Allâh (سبحانه وتعالى) Peke yake na Rehma na Amani zimfikie Mtume Muhammad (صلي الله عليه وسلم) ambaye hapatakuwa na Mtume mwengine baada yake.

Uzinifu huleta ufisadi mkubwa na hueneza uovu kwa urahisi. Madhara makubwa yanayotokamana na uzinifu husababisha maafa makubwa kwa wale wanaofanya uzinifu na kwa Ummah wa Ki-Islamu kwa ujumla. Kwa sababu yakuwa madhambi haya yameenea kwenye sehemu mbali mbali, na kwa sababu kuna njia nyingi zenye kupelekea huko, matokeo yake mabaya na uharibifu wenye kutokamana nao [huo uzinifu] ni lazima yajulikane. Kwahiyo, uzinifu husababisha yafuatayo.

*Mkusanyiko wa tabia zote mbovu na kudhoofisha imani, vilevile hung'oa ihsani na wivu na kufisadisha muruwa na kufuta wema.

*Huuwa haya na kuwafanya watenda hayo kuwa watovu wa haya.

*Hufanya uso wa mtu ukawa mweusi usio nawiri kwa wanaouangalia.

*Hutia giza nyoyo na kuikosesha nuru.

*Huleta mateso na ufakiri wenye kuendelea, kama asemavyo (سبحانه وتعالى) katika hadeeth Qudsi:

"Nitawaangamiza mabepari na nitawapa wazinifu ufakiri."

*Humfanya mzinifu kuwa hana maana mbele za Allâh (سبحانه وتعالى) na kumfanya akose heshima na thamani mbele za wanaadamu.

*Humfanya mzinifu kutojulikana kwa sifa njema na mwenye heshima na badala yake akawa atajulikana kwa sifa ya mzinzi, 'Aasi, na mtu wa khiyana.

*Humsababisha mzinifu asiwe mkundufu (asiwe na furaha), Allâh (سبحانه وتعالى) hulitia hili nyoyoni mwao na hulidhihirisha nyusoni mwao. Ambapo watu wa heshima huwa na nyuso za furaha (michangamfu) na nyoyo za furaha, na yeyote akaae nao hufurahika pamoja, jambo ambalo ni kinyume kabisa na wazinifu.

*Huwafanya watu waamiliane naye kwa shaka na kutomuamini.

*Mambo huwaendea kinyume na vile wazinifu walivyotarajia na hatimae kuwafanya wawe na huzuni. Yule atafutae starehe kwa kumu'asi Allâh (سبحانه وتعالى) (ataadhibiwa kwa kupata kinyume cha aliyoyatarajia. Mema yaweza kupatikana tu kwa kumtwi'i Allâh (سبحانه وتعالى), kwani Allâh (سبحانه وتعالى) hakufanya njia ya kupata mazuri ni kumuasi yeye. Lau kama wazinifu wangelijua starehe ipatikanao kwa kutokuwa mzinifu, watazinduka kuwa walioyakosa ni bora zaidi ya starehe walioipata kwenye zinaa.

*Wazinifu watakosa fursa ya kustarehe na wanawake wa peponi.

*Hupata hima mzinifu ya kukata kizazi na familia, akapata pato la haramu, na kunyanyasa watu na akapoteza familia yake. Haya hutokea baada ya kufanya madhambi mengine ambayo yaelekeza huko, na yasababisha madhambi mengi kutokea.

*Kuharibu heshima ya mwanamke na kumletea aibu kwake na kwa familia yake.

*Izara ya matokeo ya uzinifu kwa Muislamu ni mbaya zaidi kuliko kwa yule ambaye alifanya hivyo akiwa ni kafiri, kwa sababu pindi anaposilimu kafiri na akawa Muislamu wa kweli, Izara yake yamuondokea na huwa yuko huru kwa Allâh (سبحانه وتعالى) na mbele ya macho ya watu vilevile. Hali hii ni kinyume cha mzinifu Waislamu ambao hufutiwa dhambi yao wakitubia, lakini waangaliwa kuwa wana daraja ya chini kuliko wale Waislamu ambao wamedumisha 'Izza na heshima zao na ambao hawajafanya uzinifu. Ikiwa mtu atatizama katika jamii atapata yakwamba wale wanawake waliozini, inakuwa ni vigumu kwao kupata waume wakuridhisha.

*Ikiwa mwanamke amezini kisha akaitoa mimba atakuwa amefanya madhambi mawili makubwa. Akiwa ameolewa na akadanganya kuwa mtoto ni wamumewe, atakuwa ameleta ajnabii nyumbani ambaye akibalighi atawaona ahli wa nyumba ambao ki-Islamu hafai kuwaona bila ya hijaab; atakaa nao faragha na awarithi haliyakuwa ni makosa kisheria na vilevile kufanya madhambi mengi mengine bila ya kujua.

*Kuleta katika Ummah wa Ki-Islamu

MABAYA YANAYOPATIKANA KUTOKAMANA NA UZINIFU

mwana atakaekosa walezi na jamaa ambao watamfunza na kumuongoza wakati akiwa anakuwa ki-Umri. Zaidi ya hayo, kijana huyu (mwanaharamu) ataishi maisha yake akijihisi dufu na mwenye daraja ndogo kuliko wengine kwenye jamii.

*Waume wanaozini huharibu 'Izza ya wanawake ambao awali walikuwa wasafi na uchafu huo [wa zinaa] na hili laweza kuwatia kwenye uzinzi (uzinifu).

*Uzinifu waanzisha uadui na kuwasha moto wa kulipiza kisasi kwa familia ya mwanamke, kwa sababu ya izara watakao hisi jamii ya mwanamke baada ya dhambi hizo. Na kuzidi wivu ni jambo la kawaida kwa wana-adamu. Sa'd Ibn 'Ubaadah (رحمه الله) alisema: "Nitakapomuona mtu na mke wangu nitamkata kwa upanga wangu". Na alipoyasikia Mtume (صلي الله عليه وسلم) maneno hayo, akaongezea na kusema: "Mwastaajabishwa na wivu wa Sa'd? Naapa kwa jina la Allâh, mimi nina wivu zaidi yake na Allâh ana wivu kuniliko mimi, na wivu wa Allâh ni juu ya madhambi yanayotendwa hadharani na kwa siri." (al-Bukhari & Muslim).

*Inakuwa rahisi kwa mwanamke mzinifu kufanya kitendo hicho tena baada ya kugunduliwa mambo yake. Ikiwa malezi yake hayana misingi ya ki-Islamu. Kwa upande mwengine, yule anayejizuia na uzinifu na kukataa kwa nafsi yake na kwa wengine hupata heshima kutokamana na hayo na hili humwezesha kudumisha heshima ya nyumba yake.

*Magonjwa mengi yapatikanayo ambayo yasiyowezekana kutibika na yaweza hata kusababisha kifo, kama vile Ukimwi, visonono, gonoria na magonjwa mengine ya ngono.

*Kuagamia kwa Ummah wa Ki-Islamu kutokamana na Adhabu na hasira za Allâh (سبحانه وتعالى) juu ya watu kwa ujumla. Ibn Mas'ud (رضي الله عنه) alisema: "Inapoenea zinaa na ikaenea kijijini, Allâh huamrisha kiangamizwe." Kinachoshuhudisha kuwa uzinifu ni madhambi makubwa, ni kule kuwa Allâh (سبحانه وتعالى) ameweka hukmu maalumu kwa wenye kuyafanya hayo.

Imaam Ibn al-Qayyim (رحمه الله), alisema: "Allâh ameweka hukmu ya uzinifu iwe tofauti katika njia tatu: Ya kwanza ni adhabu ya kifo pale inapostahiki na yatekelezwa kwa njia iliyokali kabisa. Ya Pili nikuwa Allâh amewakataza waja wake kuwa na huruma na wazinifu wakati wanapowaadhibu, na Ya Tatu Allâh ameamrisha waadhibiwe hadharani mbele ya halaiki ya waumini bila ya kufichwa, na kuna hikmah kubwa katika hili kwa vile inawasababisha wengine kujikataza maasi hayo ya uzinifu."

Ni faida kutaja tofauti zilizopo katika wazinifu: Mwenye kuzini na wengi sikama anaezini na mmoja katika uovu wao, na yule anaezini kisha akaficha si mbaya kuliko anezini hadharani, kuzini na aliyeolewa ni vibaya zaidi kuliko na yule ambaye hajaolewa, kwa kuwa hilo lakiuka haki za wengine na kuwaharibia maisha yao ya ndoa.

La zaidi ni kwamba kuzini na mke wa Jirani ni vibaya mno kuliko na mwanamake asiyekuwa wa Jirani, kwa wanao fanya hivyo wanawaletea madhara majirani zao na kuvunja amri ya Allâh (سبحانه وتعالى) na Mtume Wake (صلي الله عليه وسلم) kuwa msiwadhuru majirani. Vilevile kuzini na mke wa mtu aliyekwenda kupigana Jihaad si kama kuzini na mke wa mtu mwengine.

Kama ambavyo madhambi ya zinaa yana viwango mbalili mbali kulingana na unaelala nae, pia iko tofauti kulingana na wakati na sehemu kitendo kinapofanywa. Yule anaezini mwezi wa Ramadhan si kama yule anaezini nje ya mwezi huo, na anayefanya kitendo cha uzinifu mahali patukufu sikama yule anayefanya mbali na hapo.

Zinaa inayofanywa na mzee ni mbaya kuliko inayofanywa na kijana, na zinaa inayofanywa na mwanachuoni ni mbaya zaidi kuliko zinaa inayofanywa na mtu wa kawaida na tajiri mwenye uwezo wa kufunga ndoa ni mbaya zaidi kuliko asiye na uwezo wa kuowa.

NAMNA YA KUTUBIA NA MADHAMBI YA ZINAA

Baada ya kugundua uovu wa zinaa na maangamivu ya matokeo yake juu ya mtu na jamii, ni lazima tueleze kuwa toba ya kikweli ni wajibu juu ya yule aliyezini au kusaidia wengine kufanya hivyo, mtu kama huyo ni lazima pia ajute na asirudie katika uzinifu abadan.

Anaezini asijisalimishe kwa wenye hukumu na akayakiri makosa yake, yatosheleza kwake yeye kutubia kikweli kwa Allâh na ayafiche madhambi yake. Ikiwa anapicha, au video, au kanda na mengineyo na aviangamize vyote hivyo na ikiwa amewapa wengine basi ajaribu kadiri ya uwezo wake kuvipata na kuviangamiza.

Mwanamke ambaye amezini na asikome na kutubia kwa sababu fulani alimrikodi akifanya hayo: Ni lazima aharakishe kutubia wala asijiwekee kuzuizi chochote kutokamana na vitisho vya kusalitiwa, kwa sababu Allâh (سبحانه وتعالى) atosheleza kuwa ni Mlinzi. Ni lazima aelewe kuwa anayemtisha ni muoga na itakuwa ajidhihirisha nafsi yake anapoeneza kanda hizo. Ni lipi lililo rahisi kudhihirishwa mbele za watu kwa muda mfupi? Ni kwenye maisha haya na ukawa toba yako imetakabaliwa au kesho akhera mbele ya viumbe vyote kisha wende motoni kuishi humo?

Yasisitizwa kuwa ni vyema akitafuta msaada kutoka kwa mtu mwenye busara miongoni mwa mahrimu zake, ili waweze kumsaidia kujitoa na janga hilo ovu.

(Endelea kutoka Ukurasa wa 2)

MWISHO:

Watu ni lazima watubie na kukoma na uzinifu na wavunje uhusiano na mambo yote yatakayo kuwakumbusha na madhambi hayo, ni lazima wanyenyekee kwa Allâh, na huenda Allâh akawatakabalia toba zao na kuwasamehe. Na kuwabadilishia madhambi waliyoyatenda kuwa matendo mema. Allâh **(**سبحانه وتعالى**)** amesema "**Na ambao hawamuombi pamoja na Allâh, mola mwengine na hawaiui nafsi alioiharamisha Allâh ila kwa haki na wala hawazini. Na atakayelifanya moja kati ya yaliyotajwa ataikuta (Akhera) adhabu* Atazidishiwa adhabu siku ya kiyama na atakaa humo (katika adhabu) milele ilhali ni dhalili* Ila atakayetubia (kabla hajakata roho) akaamini na akayafanya mema basi hao atayabadilisha Allâh maovu yao (ayafanye) mema na hakika Allâh ni Mwingi wa Msamaha Mwenye huruma"** [FURQAAN :68-70]

NENO LA BUSARA

قَالَ رَسُولُ اللَّهِ

صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ

الْمُتَشَبِّعُ بِمَا لَمْ يُعْطَ كَلَابِسِ ثَوْبَيْ زُورٍ

"MWENYE KUJIFANANISHA NA MAMBO AMBAYO HAKUPEWA NI KAMA MTU ALIYEVAA MAJOHO MAWILI YA URONGO."

Imepokewa na Bukhaari na Muslim.

KUKUBALI KUWA LOLOTE ASEMALO FULANI NI SAWA NA LOLOTE ASILOLISEMA SI SAWA !!?

Mtayarishi: Sheikh Swaalih Aali Sheikh

Katika misiba ya nyakati hizi ambayo iliyowasibu watu ni kwamba kunapatikana miongoni mwa watu wenye imani ya kupindukia mipaka na mapenzi ya kupita kiasi kwa wale walioghurika nao. Kwa hivyo utaona mtu haswa katika vijana, ikiwa ameghurika na mtu mwenye athari kubwa au asokuwa na athari yoyote kwa waislamu, atakuwa na mapenzi ya kupindukia mipaka juu yake bila ya haki ambapo hatasikia wala kukubali lolote kinyume nae. Hii ni aina ya **GHULUW** ambayo hairuhusiwi kwa mu'min kuwa nayo. Bali maneno yake yafaa kupimwa kwa kuwa yeye ni mtu na mfuasi wa Mtume Muhammad **(** صلي الله عليه وسلم**)**. Kwahivyo yote yanayokubaliana na Sunnah na uongofu (Qur'an) yanafaa kuangaliwa na kukubaliwa na yote yasiokubaliana nayo yafaa yakataliwe. Kwanini isiwe hivyo wakati Imam Malik **(** رحمه الله**)** amesema "Hakuna miongoni mwetu isipokuwa maneno yake huenda yakakubaliwa au yakakataliwa, isipokuwa kwa yule aliye kwenye kaburi hili (yaani Mtume **(** صلي الله عليه وسلم**)**. Kwahivyo yoyote asiyekuwa Yeye **(** صلي الله عليه وسلم**)**, basi maneno yake yanakubaliwa na kukataliwa. Hii yamaanisha kuwa haifai kuwe na mapenzi ya hawaa na upofu kutoka kwa kundi lililomzungukaka "**SHEKHE**" ambae wameghurika naye. Ikawa yachukuliwa kuwa yote ayasemayo ni sawa na asiyoyasema si sawa. Vilevile tusiwe na machukivu ya hawaa na upofu ambapo mambo yote mwanachuoni au mwanafunzi wa ki-Ilimu anapokuwa sawa nayo yakataliwa na kupinduliwa. Bali ni wajibu kusema kwa yule aliyefanya vyema "umefanya vyema", na kusema kwa yule aliopata "umepata", na kwa yule aliokosa "umekosa"- hili ndilo lililo la wajibu juu ya waumini. Sio wafumbe macho yao na nyoyo zao na wakawa wafuasi wa kila kitu kutoka kwake yule waliye na fanaa naye (mahaba ya usufi), awe sawa au asiwe sawa. Hili lataka lipewe malezi ya kulifanya la muhimu na ni malezi yanayotakiwa yapewe kipa-Umbele katika nyoyo za waumini- na ndiyo Manhaj isiyo na kosa kwa mategemezi ya ushahidi usio na upungufu: Kitâb, Sunnah na ijmaa' ya Ahl us-Sunnah wal-Jama'ah na muafaka uliotajwa kwenye Aqeedah yao. Kwa asiyekuwa na sifa hizi, basi anafaa aangaliwe kulingana na 'Ilmu aliyonayo na uongofu wake. Hili ni jambo muhimu ambalo vijana wanafaa wafungue nyoyo zao wala wasizizuie nyoyo zao na wakaweka maoni mbele ya Kitâbu na Sunnah, HAPANA! **Kwa kuwa hapana mtu yoyote isipokuwa maneno yake ni ya kukubalika au kukatalika na nia sikuamini kuwa aliye sawa ni maasoom na yule ambaye maneno yake hayako sawa abwagwe kabisa, HAPANA! Bali kila mtu aungamane baina ya kuwa sawa na kutokuwa sawa**. Kwahivyo, yule aliyesawa afaa kufuatwa kwa lile alilokuwa sawa kwalo, isichukuliwe kuwa amemiza usawa wadaima, bali afaa amulikwe kwa lile alilokuwa sawa nalo na asifiwe kwa usawa huo. Vilevile yule anayekosa nae akataliwe na isemwe "umekosa katika hili" na asifuatwe katika makosa yake na katika alilokosa lisifuatwe. Hii ndio Manhaj iliyo swaheeh katika mas'ala haya kuhusu anayekosa juu ya mas'ala ya ijtihad. Kwahivyo tusipite mipaka wala kupuuza kwa kuwa kupitisha mipaka na kupuuza yakatazwa miongoni mwa Ahlu-uSunnah wal-Jama'ah. Kwahivyo ni lazima, bali ni wajibu hili liwenasi: Ili tukataze ghuluu zisiwe katika hali za watu, 'Ulamaa' na watu wema, hii ndiyo kaida ya Ahl us-Sunnah wal-Jama'ah. Ghuluu ni katika asili ya mambo ya ki-Jâhiliyyah kwa sababu ndiyo inayoleta mahaba ya upotofu ambapo roho hukiri jambo na kughurika na mtu kwa kiasi cha kuwa maneno ya "SHEKHE" yanakuwa ni maneno yake hata ikiwa ni makosa kutoka kwa "SHEKHE".

Na Sheikh Muhammad Bin Swaalih al-Munajjid.

Jirani yangu wa kike ni mkristo wa Ki-America, nae na familia yake walininunulia zawadi siku ya Christmas. Sikuweza kuikataa zawadi ile ili asje akaona vibaya. Naweza kukubali zawadi kama hii kama alivyokuwa akikubali zawadi Mtume (صلي الله عليه وسلم) kutoka kwa makaafir?

AlhamduliLLah:
Kwanza amri ya kawaida ni kuwa yakubaliwa kutwaa zawadi kutoka kwa makaafir ili kulainisha nyoyo zao na kuufanya Uislamu uvutie kwao, kama alivyokubali Mtume (صلي الله عليه وسلم) zawadi kutoka kwa al-Muqawqis na wengine. Al-Bukhari (رحمه الله) ameweka mlango katika swaheeh yake: "Kukubali zawadi kutoka kwa Mushrikeen". Naye (رحمه الله) akasema: Abu Hurayrah (رضي الله عنه) alisema, akihadithia kutoka kwa Mtume (صلي الله عليه وسلم) alisema: "Ibraheem (عليه السلام) alihama na Sara na wakaingia kwenye mji ambao ulikuwa na Mfalme jabari, akasema (mfalme) mpe Haajar (kama zawadi)." Na Mtume (صلي الله عليه وسلم) alipewa zawadi kondoo wakuchomwa mwenye sumu. Abu Humayd alisema: "Mfalme wa Aylah alimpa Mtume (صلي الله عليه وسلم) nyumbu mweupe na kishale, na akaandika kisa cha mwanamke wa kiyahudi aliyempa Mtume (صلي الله عليه وسلم) kondoo aliyetiwa sumu.

PILI: Yaruhusiwa kwa Muislamu kuwapa makaafir na mushrikeen zawadi ikiwa lengo ni kulainisha nyoyo zao waingie kwenye Uislamu haswa wakiwa ni jamaa au majirani.

Umar (رضي الله عنه) alimpa Hullah (suit) ndugu yake mushrik kama ilivopokewa na al-Bukhari (رحمه الله)

Lakini haifai kumpa kaafir zawadi siku za sherehe zao, kwa sababu hilo latukuliwa kuwa waridhia au kushiriki katika sherehe zao. Ikiwa zawadi ni vitu vitakavyo kusaidia sherehe kama chakula, mishumaa, na mifano kama hiyo basi ni haraam zaidi na baadhi ya maulamaa wasema kuwa hii ni kufru.

NASWAHA YA MUHADDITH WA MADEENAH AL-ALAMAH SHAYKH MUHSIN AL-ABAAD AL-BADR (حفضه الله)

KWA WANA FUNZI WAILMU AM-BAO WAFANYA PUPA KUWAHU-KUMU WENGINE BILA YA HAKI

SUALA: Unayo naswaha yoyote kwa baadhi ya wanafunzi wa 'Ilmu wenye kufanya haraka katika kupitisha hukmu juu ya wengine na kuwawajibishia yale ambayo hayafai kuwajibishwa na kuyapanua mas'ala yenye kuzidisha tafauti na hatimae kuzidisha tofauti zilizoko? Na baadhi ya mas'ala haya ambayo ndani yake yaweza kukaweko na maoni tofauti, bali ndani ya mas'ala haya baadhi ya wanafunzi huzidisha katika kutuhumu wapinzani wao na huenda yakaenea mpaka katika mitandao na baadaye kukasababishwa fitnah baina ya wanafunzi.

JIBU: Ni wajib kwa kila Muislamu, na wanafunzi wa dini, kumcha Allâh (سبحانه وتعالى) na kujishughulisha na kupata 'Ilmu na kupata kuijua njia moja au nyingi ambazo Kibaar 'Ulamaa (wavyooni wakubwa) walizipitia njia hizo kama vile Mashaykh Binbaaz, Ibn 'uthaymeen, Shinqeetee, na al-Albaanee (رحمهم الله) Kumaanisha kuwa mtu apaswa kulinda na kujua yale ambayo Kibaar 'Ulamaa walikuwa juu yake katika kujishughulisha na 'Ilmu. Ama kuhusu hali ya mtu kuwa ameshughulishwa na "Qeela Wa Qaal" na kufuata makosa au kutafuta makosa na kuonya watu juu ya yale anayoyapata kuwa 'ana kadha na ana kadhaa'. Kujishughulisha na haya huwafanya watu kukaa mbali na 'Ilmu na huwashughulisha na yale yasiowaletea faida. Mtu atakiwa alinde na kuhifadhi 'Ilmu na kufaidika nayo na kushughulishwa nayo. Na ikiwa kosa limetokea kwa mtu, ikiwa yeye ni katika Ahl us-Sunnah na katika wale walio shughulika na 'Ilmu, basi mtu kama huyo hafai kutupwa wala watu kupewa onyo kumuhusu yeye. Bali yafaa watu wafaidike naye na wajue kuhusu kosa lake na vile vile kosa lake lafaa kuonywa watu. Ama kuhusu yeye kutupwa na kuwekewa vikwazo na kutolewa onyo kumuhusu yeye basi hii si njia ya uadilifu wala ya kupata 'Ilmu. Kwa sababu Ahl us-Sunnah wakiwa katika njia hii itamaanisha kidogo kidogo wapotea na hakuna atakaebakia kulingana na misimamo yao. Kwahivyo ni juu ya mtu kuhifadhi na kupata 'Ilmu na kushughulishwa na 'Ilmu na asije akashughulishwa na qeela wa qaal (maneno ya uvumi) kwani hao wanaoshughulika na mambo hayo hawapati 'Ilmu wala hawashughuliki na 'Ilmu wanashughulika tu na qeela wa qaal. Hakuna faida inayopatikana na kutoka kwa hayo ila madhara ndiyo yanayotokea kwa kuwazungumza wengine. Kushughulishwa na mas'ala haya yasiyo na faida yasiyostahiki mtu kushughulishwa nayo, na yasiyostahiki mtu kupoteza wakati wake nayo, ambayo yakata njia za kufaidika kutoka kwa wengine na walioshughulika na 'Ilmu.

JEE YAPITA TALAKA ILIYOKO MOYONI? Sheikh Ibn Baaz (رحمه الله)

Nilikuwa na utesi na mke wangu na baada ya ugomvi, nikasema ndani ya nafsi yangu, bila ya kutamka maneno: 'Kwanini simwambii: 'Nimekutaliki'? Kuna jambo lolote linalosimama juu yangu kwa sababu ya fikra nilizokuwa nazo ingawa sikutamka? Nipe hukmu na Allâh atakujazi wema.

JAWABU: Ikiwa hali ni kama ulivyoieleza katika suala, basi talaqa iliyokusudiwa haihesabiwi, kwa sababu talaqa ya niya pekee haimo.Talaqa huhesabiwa kwa kauli au maandishi, kulingana na maneno ya Mtume (صلي الله عليه وسلم): "Hakika Allâh hachukulii (hahesabu) kwa Ummah wangu mambo yaliyomo ndani ya nafsi zao mpaka watende au watamke" (Imepokewa kutoka kwa Abu Hurayrah (رضي الله عنه) [al-Bukhari & Muslim).